

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



Dar es Salaam
28 Juni, 2026

Barua pepe: press@ikulu.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

RAIS SAMIA, DANGOTE WAJADILI FURSA ZA UWEKEZAJI NCHINI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo amekutana na kufanya mazungumzo na Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Dangote Group, Alhaj Aliko Dangote, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Dangote, ambaye ni mwekezaji na mfanyabiashara kinara barani Afrika, ameeleza utayari wa kampuni yake kupanua ushirikiano wa uwekezaji na Serikali katika sekta mbalimbali za kimkakati.

Mazungumzo hayo yamegusa maeneo ya miundombinu ya usafirishaji, uzalishaji wa mbolea nchini na nishati, kama sehemu ya fursa za uwekezaji zinazoweza kuchochea shughuli za kiuchumi nchini na katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Dangote amesema Tanzania ina mazingira mazuri ya uwekezaji na fursa kubwa za kukuza viwanda vinavyoongeza thamani ya malighafi na kuchochea biashara ya kikanda.

"Tumetambua maeneo yenye manufaa makubwa kwa Tanzania na tuko tayari kushirikiana na Serikali kuyaendeleza kwa manufaa ya pande zote," amesema Dangote.

Kwa upande wake, Rais Dkt. Samia amesema Serikali imepokea nia hiyo na kuzielekeza wizara na taasisi husika kuendelea na majadiliano ya kitaalamu kuhusu maeneo yaliyojadiliwa, kwa kuzingatia sera, sheria na vipaumbele vya maendeleo ya nchi.

Amesema Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuvutia uwekezaji wenye tija unaochochea ukuaji wa uchumi, maendeleo ya viwanda, uhamishaji wa teknolojia na ajira kwa Watanzania.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu



[Ikulu Mawasiliano / ikulu_mawasiliano /](#)
[ikulu_Tanzania / ikulu_Tanzania /](#)
[ikulumawasiliano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania](#)

